

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

01

KISWAHILI

Muda Saa 1:30

Mwaka: 2021

Maelekezo

1. Mtihani huu una sehemu A, B, C, D na E zenyе jumla ya maswali **matano (5)**.
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.
3. Sehemu A, B, C, D na E zina alama **kumi (10)** kila moja.

SEHEMU A: (Alama 10)

1. Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

(vi) _____
(vii) _____
(viii) _____
(ix) _____
(x) _____

SEHEMU B (Alama 10)

2. Katika kipengele (i) – (ii), andika wingi wa maneno yafuatayo kwa kuandika jibu sahihi kwenye nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Mto _____
(ii) Ukucha _____
(iii) Ng'ombe _____
(iv) Ufa _____
(v) Wembe _____

SEHEMU C (Alama 10)

3. Andika jibu sahihi kwa maswali yafuatayo:

(i) Bibi hulalamika kila siku anaibiwa fedha zake, siku moja alimkutta Chautundu anaiba fedha zake. Bibi atatumia methali ipi kumsuta Chautundu? _____

Utatumia methali ipi kumhimiza rafiki yako kufanya kazi kwa bidii?

“Samaki mkunje angali mbichi” Methali hii ina maana gani?

(ii) Kamilisha methali zifuatazo kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi:
(a) Mdharau mwiba _____

(b) Kilema si _____

SEHEMU D: (Alama 10)

4. Weka alama za uandishi katikasentensi zifuatazo kwa kuandika alama sahihi katika nafasi ilioachwa wazi.
- (i) Afadhalii _____ mgeni amewasili _____
 - (ii) Baba ameninunlia kalamu _____ rula na daftari _____
 - (iii) Hodii _____ je wenyeji wangu mpo _____
 - (iv) Aka _____ mimi sipendi utoro _____
 - (v) Mama _____ baba na kaka watasafiri kesho _____

SEHEMU E: (Alama 10)

5. Soma kwamakini kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi ilioachwa wazi.

Hapo zaman za kale Kanga na Kuku walikuwa marafiki sana. Wote waliishi kwa binadamu. Kuku alikuwa na tabia ya uchoyo. Kuku alikuwa na sindano nzuri ya kushonea nguo. Kila siku Kanga alipojaribu kuazima sindano, Kuku alikataa katakata. Siku moja Kanga aliiba sindano ya Kuku akaenda kuificha porini.

Kuku aliporudi aliitafuta sindano yake kila mahali lakini hakuionna. Alianzisha ugomvi mkubwa sana. Wakati wanapigana, Kuku alichukua kalamu mezani kasha akampigia Kanga. Kwa bahati mbaya wino wa kalamu ulivuja mpaka ukaisha. Ndiyo maana hadi leo Kanga ana madoamadoa na Kuku anaparua ardhini kutafuta sindano yake.

Maswali:

- (i) Kuku na Kanga waliishi wapi?
- (ii) Nani alikuwa na sindano ya kushonea nguo? _____
- (iii) Sindano ilipoibwiwa ilifichwa wapi? _____
- (iv) Hadithi hii inahusu nini? _____
- (v) Hadithi hii inatoa funzo gani? _____